



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO

*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na.HA.92/243/01/65

Tarehe: 29 Agosti, 2025

Mkurugenzi Mkuu,

Mamlaka ya Uwekezaji na Ukanda Maalum wa Kiuchumi (TISEZA),

S.L.P 938,

**DAR ES SALAAM.**

Yah: **OMBI LA KUTOKUWA NA PINGAMIZI LA UTOAJI WA CHETI CHA UWEKEZAJI  
KATIKA KIWANJA NA. 451 KITALU "A" ZINGA WILAYA YA BAGAMOYO**

Tafadhali husika na kichwa habari hapo juu.

2. Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo imepokea barua yenye **Kumb.Na.ITZ/HQ/DSM/0077** ya tarehe **20 Julai, 2025** kutoka Kampuni ya Irvine's Tanzania Limited ya kuomba kupata barua ya kutokuwa na pingamizi kwa mradi utakaofanyika katika kiwanja tajwa ili Ofisi yako iweze kutoa Cheti cha Uwekezaji.
3. Vilevile, barua hiyo imeeleza kuwa, walipofuatilia ili kupata Cheti cha Uwekezaji katika Ofisi yako walielekezwa kupata kwanza barua ya kutokuwa na pingamizi la uwekezaji kutoka Halmashauri. Aidha, Kampuni hiyo imewasilisha nakala ya mkataba unaonyesha Kampuni hiyo imenunua eneo la kiwanja tajwa kutoka Kampuni ya Future Century Limited.
4. Kulingana na kumbukumbu za Ofisi, kiwanja tajwa kinatokana na mgawanyo wa kiwanja **namba 1 kitalu "A" Zinga** ambacho kilikuwa kinamilikiwa na Kampuni ya Future Century Limited kabla ya kurejesha miliki hiyo Serikali ili kupisha mgawanyo huo.

5. Hivyo, Ofisi haina pingamizi kwa uwekezaji utaofanyika katika kiwanja tajwa kwa kuzingatia matumizi yaliyoainishwa katika mchoro wa Mipangomiji wa eneo husika pia, Kampuni hiyo itapaswa kukamilisha taratibu za kupata umiliki kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 na Sheria ya Uwekezaji Tanzania kwakuwa Kampuni hiyo ni ya kigeni.

6. Ahsante.



Shauri Selenda  
**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**  
**BAGAMOYO.**

**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**  
**BAGAMOYO**  
**S.L.P. 59**  
**BAGAMOYO**

Nakala:- Mkurugenzi,  
Irvines Tanzania Limited,  
S.L.P 39997,  
**DAR ES SALAAM.**

– Kwa taarifa

Mkurugenzi,  
Future Century Limited,  
S.L.P 301,  
**BAGAMOYO.**

– Kwa taarifa